**Sikiliza na Ujifunze**

**( Wapinzani wa Utandawazi : Globalisierunsgegner )**

**M.Dahman (HON)**

---

**3 Stimmen : Sauti 3 :**

- **Msemaji kijana wa kiume**
- **Msemaji kijana wa kike**
- **Msemaji wa kike 2 kwa Repoti : als Off _Stimme für die**
- **Reportage**
- **------------------------------**
- **Für die O-Töne dazu . Sauti za O-Töne**
- **1 junge Frau ; Mwanamke kijana**
- **1 Frau : Mwanamke**
- **2 Männer : Wanaume wawili**
- **---------------------------------------**

**Vorspann LbE**

**TEIL 1 : SEHEMU YA KWANZA REPOTI**

**Msimulizi wa kike 1 :**

**Habari gani! Natumai nyote hamjambo !**

**Msimulizi wa kiume 1:**

**Leo katika mfululizo wa vipindi vyetu vya utandawazi tutazungumzia juu ya watu wanaopinga utandawazi…..**

**Msimulizi wa kike 1 :**

**Dhidi ya utandawazi ! Watu wanaopiga kampeni kwa ajili ya aina tafauti ya utandawazi.**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Tutatembelea radio moja ya jumuiya inayopinga utandawazi nchini Niger.**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Na tunaelekea katika mji mkuu wa nchi hiyo Niamey !**

**Msimulizi wa kiume 1 na wa kike 1 :**

**Kwa hiyo fungeni mikanda yenu tayari kwa safari !**

**…………………Manuscript :…………………….**

**1.Globalisierung Gegner : Dhidi ya Utandawazi (Frauenstimme ….. Sauti ya kike)**

**'Studio ya Ernesto Che Guevara ---kwa vile alikuwa ni mtu aliepigania mabadiliko katika dunia hii---Radio Mbadala inachotaka kufanya ni kufunguwa milango ya kipindi cha usoni kwa kufanya vile vile kama alivyofanya Che Guevara'**

**Msimulizi wa kike 2 :**

**Mwanamapinduzi huyo wa Argentina ni mojawapo ya mfano wa kuigwa unaotumiwa na radio ya FM Mbadala ……radio hiyo ya jumuiya ina maelfu ya wasikilizaji vijana mjini Niamey na karibu na mji huo. Imeanzishwa hapo mwaka 1994 na hasa inawalenga vijana na wanawake kwa kupigania maendeleo.Assane Boka mwandishi habari na mkurugenzi wa zamani wa radio hiyo anajivunia sifa za radio hiyo za kupinga utandawazi.**

**2 . Globalisierung Gegner 2 …….Dhidi ya Utandawazi**

**``Tumeshiriki katika mikutano ya Mabaraza ya Kijamii Duniani.Radio ni njia ya kuwaelezea watu vuguvugu hili linamaanisha nini.Kwa kuwaeleza watu kwa nini tunajihusisha na kwa nini vijana wanapaswa kujihusisha katika vuguvugu la kupinga utandawazi `.**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Baraza la Kijamii ni kitu gani ?**

**Msimulizi wa kike 1 :**

**Ni mkutano wa kila mwaka unaofanywa na wanachama wa vuguvugu la kupinga utandawazi kuratibu kampeni za dunia na kujulishana juu ya harakati zao na masuala ya utandawazi.Hapo maka 2007 Baraza la Kijamii Duniani lilifanyika mjini Nairobi mji mkuu wa Kenya .Kauli mbiu ya Baraza la Kijamii Duniani ni Inawezekana kuwa na Dunia Aina Nyengine .Wapiga kampeni wanasema siasa na uchumi zinaweza kuendeshwa tafauti.**

**3 . Globalisierung Gegner Atmo 1 (Sendemitschnitt)……**

**Msimulizi wa kike 2 :**

**Takriban vipindi vingi vya radio FM Mbadala huwa vinaelezea jinsi utandawazi unavyofanya kazi. Vipindi hivyo huyalaumu mashirika ya kimataifa kama vile Shirika la Biashara Duniani WTO,Shirika la Fedha la Kimataifa IMF na Benki ya Dunia kwa kuendeleza mfumo usio wa haki. Vipindi vyengine huwa zaidi juu ya masuala ya ndani ya nchi . Fada Mbadala ni kipindi kinachoingiliana na masuala ya kijamii kinachotangazwa kwa lugha ya Djema inayozungumzwa na watu milioni mbili katika bonde la Mto Niger.**

**4. Globalisierung Gegner 3 - Frauenstimme : Sauti ya Kike**

**´ Katika kipindi cha Fada Mbadala tunazungumzia matatizo ya kijamii.Hatujuwi kwa nini Wanigeria hulalamika. Daima wanasema kuwa wao ni maskini lakini pale wanapoandaa kitu kwa mfano harusi,kubatiza au mazishi inabidi wawe na karamu kubwa …chakula,mambo ya mila na kadhalika.Kwa nini watumie gharama kubwa ?**

**Msimulizi wa kike 2 :**

**Radio FM Mbadala inaamini kwamba ili kuweza kuibadili dunia kwanza inabidi ujibadili mwenyewe binafsi.Mama Sani ni mwalimu wa biolojia na mwanachama hai wa**

**vuguvugu dhidi ya utandawazi nchini Nigeria.Ana mashaka na mashirika ya kimataifa.**

**5.Globalisierung Gegner Atmo 2 (Schritte u.Stimmen)**

**6. Globalisierung Gegner 4**

**` Hakuna rasilmali yetu yoyote ile inayonunuliwa kwa bei ilio sawa.Na iwe madini ya uranium au dhahabu wanayapora tu na hatuwezi kusema hali hii itaisaidia Niger kuondokana na hali ya maendeleo duni iliokuwa nayo. Inabidi tuwe na bei zilizo sawa kwa mali ghafi zetu ili taifa liweze kuwa na mapato ya kutosha kuwekeza katika sekta ya jamii ….katika elimu,maji ya kunywa, miundombinu …….Sekta binafsi haiwezi kufanya hayo …hakuna fedha za kujengea barabara.Sekta binafsi itatoza tu kodi kwa kila gari linalopita barabarani…..**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Huwa wanashutumu na kushutumu lakini nini hasa wanachokitaka ?**

**Msimulizi wa kike 2 :**

**Assane Boka anaelezea :**

**7. Globalisierung Gegner 5**

**- 6 –**

**Tunahtaji kuwa na mchakato wa utandawazi wenye kuheshimu haki za binaadamu.Tunahitaji mchakato wa utandawazi wenye kuruhusu binaadamu wote katika dunia kufaidika kutokana na maarifa ya kisayansi,kufaidika na utajiri wa dunia hii.Angalia ruzuku za pamba nchini Marekani …….kwa mfano Umoja wa Ulaya na Waafrina wanaheshimu sheria za Shirika la Biashara Duniani WTO wakati wanapowapa wakulima ruzuku lakini wanakwenda kinyume na matakwa ya watu na ndio maana tuna matatizo yote haya.Nchi zetu huingia mikataba na Shirika la Biashara Duniani WTO au Shirika la Fedha la Kimataifa IMF au na Benki ya Dunia ……..sisi raia inabidi tufahamu kile kinachoendelea faraghani ili kwamba tuweze kushutumu hatua zote hizi.**

**Ende Teil 1 ….Mwisho Sehemu Ya Kwanza**

**Jingle Learning by Ear**

**TEIL 2 ERKLÄRSTÜCK**

**(Nur noch Sprescher 1 Sprescherin 1 ) Msemaji wa kiume 1 na wa kike 1 tu .**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Kwa hiyo sasa unaweza ukanielezea haya hasa ni mashirika gani ………..WTO,IMF na Benki ya Dunia?**

**- 7 -**

**Msimuliz wa kike 1 :**

**Unaweza kupata habari zote kwenye mtandao.Lakini ninaweza nikakueleza kwa muhtasari……IMF ni Shirika la Fedha la Kimataifa na limekuwepo tokea mwaka 1947 . Nchi 185 ni wanachama wa shirika hili ……sawa takriban na ulimwengu mzima.**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Na huwa hasa linajishughulisha na kitu gani ?**

**Msimulizi wa kike 1 :**

**Huwa kwa kiasi kikubwa linasimamia viwango vya kubadilisha fedha baina ya sarafu tafauti na kuratibu mfumo wa fedha wa kimataifa.Husimamia ,husaidia na hutowa mikopo kwa nchi ambazo zina matatizo ili kwamba kuwepo na aina fulani ya uthabiti wa kutoyumba katika biashara ya kimataifa.**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Na vipi kuhusu WTO…..dhima yake ni nini ?**

**Msimulizi wa kike 1 :**

**Shirika la Biashara Duniani ………**

**- 8 -**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Kwangu mimi inaonekana kazi zake sawa na zile za IMF?**

**Msimulizi wa kike 1 :**

**Katika tovuti yake ya mtandao linadai kuwa ni shirika pekee duniani lenye kupanga sheria za biashara ya kimataifa. Mikataba ya WTO mara kwa mara hujadiliwa upya na kusainiwa na mataifa makubwa ya kibiashsra duniani.Kwa hiyo shirika hilo huzihusisha serikali.**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Kwa ajili gani ?**

**Ili kurahisisha taratibu za mabadilishano huru ya kibiashara ili kwamba wazalishaji na watowa huduma,wanaosafirisha nje bidhaa na wale wanaoagizia bidhaa wote waweze kufanya kazi zao.**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Kwa hiyo hizi ni kama sheria za mchezo kwa ajili ya biashara kati ya mataifa tafauti?**

**Msimulizi wa kike 1 :**

**- 9 -**

**Ndio hasa!Na Benki ya Dunia ipo kwa ajili ya kutowa msaada wa kifedha na wa kiufundi kwa nchi zinazoendelea.**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Je unaweza kuwa na akiba ya fedha katika benki hiyo na kuiombea mkopo nchi yako?**

**Msimulizi wa kike 1 :**

**Hapana ! Hiyo sio benki kama vile benki nyengine !**
**Benki hii imeundwa na taasisi mbili za maendeleo …Benki ya Kimataifa kwa ajili ya shughuli za Ujenzi mpya na Maendeleo kwa kifupi IBRD ambayo ni kwa ajili ya nchi ambazo zina utajiri wa wastani au ni maskini lakini zinaweza kulipa madeni yake na ya pili hujulikana kama ni Chama cha Maendeleo cha Kimataifa IDA kwa ajili ya nchi maskini kabisa.**

**Msimulizi wa kiume 1 :**

**Kwa hiyo kwa kutegemea na mahitaji benki hiyo hutowa au hukopesha fedha kwa riba za viwango vya chini ili kwamba isije kuharibu uchumi wa nchi hizo ambao tayari ni dhaifu…**

**Msimulizi wa kike 1 :**

**- 10 -**

**Ndio! Lakini kama tulivyokuwa tumesikia kwenye repoti, hiyo ni nadharia tu.Hata hivyo wanaharakati wanaopinga utandawazi hawakubaliani na mbinu zinazotumiwa na mashirika haya makubwa.**

**Outro………Funga Kipindi**

**Msimulizi wa kike 2 :**

**Na hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi chetu cha Sikiliza Ujifunze----Noa Bongo Jenga Maisha Yako ! Asante kwa kusikiliza kipindi hiki juu ya utandawazi na harakati dhidi ya utandawazi.Ni kipindi cha Deutsche Welle kilichotayarishwa na Habou Adi na Yann Durand.Kujuwa zaidi juu ya kipindi hiki au ukitaka kusikiliza tena tafadhali nenda kwenye tovuti yetu www.dw-world.de/lbe.**

**Usikose kujiunga nasi tena wakati mwengine ! Kwaheri !**